## 13F-Al-Waqf Al-Qabiyh (Kisimamo Kinachochukiza Au Kibaya)

### iv- الْوَقْفُ الْقَبِيح Al-Waqf Al-Qabiyh - Kisimamo Kinachochukiza Au Kibaya

Kisimamo katika neno la Qur-aan ambalo linahusiana na yanayofuatia kimaana na kilugha na kusimamia hapo kunaleta maana iliyopunguka au kosa.

**Hukmu Yake:**

Haijuzu kwa msomaji kukusudia kusimama sehemu yoyote ile katika sehemu zenye kueleweka kuwa kusimama kwake kunapelekea kuwa ni katika visimamo vibaya kabisa ila kwa dharura; kama kuishiwa na pumzi au kupatwa na kikohozi au kusahau n.k., na wakati huo msomaji atatakiwa arudie yaliyotangulia na kuyawasilisha na yanayofuatia ili maana itimie.

Kisimamo hiki ni muhimu mtu kukitambua na kukishughulikia kanuni zake kwa sababu atakaposimama mtu kwenye kisimamo hiki kauli hiyo haitakubalika kwa sababu huenda ikasababisha yafuatayo:

- Kuleta maana iliyopunguka.
- Kuleta maana isiyokusudiwa.
- Maana huenda ikawa ni ya kupotosha kabisa khasa katika itikadi sahihi.
- Huenda ikawa ni ukosefu wa adabu au itikadi potofu kuhusiana na Allaah (سبحانه وتعالى) na utukufu Wake.

### Mifano ya الْوَقْفُ الْقَبِيح Al-Waqf Al-Qabiyh - Kisimamo Kinachochukiza Au Kibaya

- Mfano wa kwanza:

  Kusimama katikati ya aayah kwenye neno ٱلصَّلَوٰةَ katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقْرَبُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنتُمْ سُكَـٰرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُواْ مَا تَقُولُونَ

((Enyi mloamini! Msikaribie Swalaah na hali mmelewa mpaka mjue mnayoyasema,))[1]

Hiki ni kisimamo cha kuchusha kwani maana haiwezi kutimia na kueleweka kama ilivyotakiwa; kwani kwa kusimama hapo inapelekea maana ibadilike na kueleweka maana isiyokusudiwa kwamba Muislamu asikaribie Swalaah bila ya kutajwa sababu yake na hali maana iliyokusudiwa ni kuwa Swalah isikaribiwe hali ya kuwa mtu amelewa ili asije kusema asiyoyatambua.

- Mfano wa pili:

Kusimama katikati ya aayah kwenye neno طَيِّبِين katika kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

ٱلَّذِينَ تَتَوَفَّىٰهُمُ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةُ طَيِّبِينَ ۙ يَقُولُونَ سَلَـٰمٌ عَلَيْكُمُ ٱدْخُلُواْ ٱلْجَنَّةَ بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٣٢﴾

((Ambao Malaika huwafisha katika hali njema watasema: [kuwaambia Waumini]: "*Salaamun 'Alaykum* [amani iwe juu yenu]! Ingieni Jannah kwa yale mliyokuwa mkitenda"))

Hiki ni kisimamo cha kuchusha kwani maana inayoeleweka kwa kusimama hapo ni maana potofu na haikubaliki, hivyo msomaji atakaposimama hapo katika neno lenye alama hiyo ya لا itapelekea kueleweka na kufahamika kinyume na inavyotakiwa ieleweke (makosa); kwani maana iliyokusudiwa ni kuwa: Malaika ndio watakaowaambia Waumini: "Salaamun 'alaykum ingieni Jannah **……**" Lakini akisimama msomaji hapo kwenye neno la طَيِّبِين kisha akaanza na kauli ya: "Watasema**…..**" huenda ikadhaniwa kuwa ni

[1] An-Nisaa (4: 43)

Waumini watakaosema kauli hiyo ya “Salaamun ‘alaykum…” badala ya kuwa ni kauli ya Malaika.

- Mfano wa tatu:

  Kusimama katikati ya Aayah kwenye neno لَا يَسْتَحْيِۦٓ katika kauli ya Allaah:

  ﴿ ۞ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَسْتَحْيِۦٓ أَن يَضْرِبَ مَثَلًا مَّا بَعُوضَةً فَمَا فَوْقَهَا ۚ

  ((Hakika Allaah Haoni *hayaa* kupiga mfano wa mbu na ulio zaidi yake [kwa udogo]….))[2]

  Hiki ni kisimamo cha kuchusha kabisa kwani msomaji akisimama katika hilo neno itapelekea kupotosha kabisa maana na kumkosea adabu Allaah (سبحانه وتعالى), kwani itabadilika na haiwezi kukubalika kabisa; kwani maana itakayoleta kusimama hapo itakuwa ni ‘Allaah haoni hayaa’ na hali ilivyokusudiwa ni kuwa: “Hakika Allaah Haoni *hayaa* kutoa mfano hata wa mbu na ulio wa zaidi yake”; ni katika muhali kumnasibisha Allaah Aliyetakasika na Kutukuka na Swiffah kama hiyo. Tunajikinga na Allaah (سبحانه وتعالى) dhidi ya makosa kama hayo.

- Mfano wa nne

  Kusimama katikati ya aayah kwenye neno وَٱللَّهُ katika kauli ya Allaah:

  ﴿...... فَبُهِتَ ٱلَّذِى كَفَرَ ۗ وَٱللَّهُ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ ٱلظَّـٰلِمِينَ ﴿٢٥٨﴾ ﴾

  ((Akapigwa na butwaa [akafedheheka] yule aliyekufuru na Allaah Haongoi watu madhalimu))[3]

  Hiki ni kisimamo cha kuchusha kabisa kwani msomaji akisimama katika hilo neno itapelekea kupotosha maana kabisa tena upotoshaji wenye kuchukiza kupita kiasi, kwani maana haitobadilika tu bali itaharibika na kueleweka maana isiyokusudiwa na ni potofu kupita kiasi; kwani maana iliyokusudiwa ni kuwa: Akafedheheka yule aliyekufuru; na ni katika muhali kuwa Allaah Aliyetakasika na

[2] Al-Baqarah (2: 26)
[3] Al-Baqarah (2: 258)

Kutukuka akawa pia Amefedheheka; hakuna katika waumini mwenye kukubali hilo, kwani hayo ni katika yenye kueleweka kuwa ni mustahili katika yenye kumhusu Allaah.

- Mfano wa tano:

  Kusimama katikati ya Aayah kwenye neno لَآ إِلَٰهَ katika kauli ya Allaah:

  ﴿ فَٱعۡلَمۡ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَٱسۡتَغۡفِرۡ لِذَنۢبِكَ وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِ....

  ((Basi elewa kwamba *laa ilaaha illa-Allaah* [Hapana mungu anayastahiki kuabudiwa kwa haki ila Allaah], na omba maghfirah kwa dhambi zako na [kwa dhambi za] Waumini wa kiume na Waumini wa kike.)[4]

  Hiki ni kisimamo cha kuchusha kabisa kwani msomaji akisimama katika hilo neno itapelekea kupotosha maana kabisa tena ni upotoshaji ulio mbaya kabisa na ni wenye kuchukiza sana; yaani kukiri kwamba "hakuna mungu" kabisa na hali kuna *istithniaa* (isipokuwa). Kusimama hapo basi, maana haitobadilika tu bali itaharibika na kueleweka maana isiyokusudiwa na ni potofu kupita kiasi na hali maana halisi na iliyokusudiwa ni kuwa: 'Elewa ya kwamba hapana mungu anayestahiki kuabudiwa kwa haki ila Allaah...

---

[4] Muhammad (47: 19)